

Kanuni Zetu za Maadili: Kwa Muhtasari

Watu na Mazingira hustawi tunapo...



Tunajitoa kwa Tunu Zetu

- Uadilifu usio na hatia
- Kuheshimu Watu, Jamii na Tamaduni
- Kujitolea kwa Utofauti
- Uhifadhi mmoja
- Matokeo yanayoonekana, ya kudumu

Maadili yetu huathiri sifa zetu kama shirika na jinsi tunavyojipambanua kama watu binafsi.

Tunaelewa Matarajio na Wajibu Wetu

Kanuni hizi zinatumiwa ulimwenguni kote kwa wafanyakazi wote wa TNC, wajumbe wa bodi, wadhamini, wafadhili, na watu wanaojitolea katika mipango yote ya TNC, vitengo vya biashara, na washirika. Ni muhimu kwa kila mtu, na tunatilia maanani ukiukaji.

Tunatarajia wadau wengine na washirika ambao tunaofanya nao biashara kutenda kwa njia ambazo zinaendana na Kanuni zetu.



Heshimiana

KUTENDA *Kitaaluma na kwa Heshima*
Katika TNC, tunaewa kuwa jinsi tutakavyokuwa hupelekea mafanikio ya juu ya wito wetu. Tunafanya kazi yetu kwa ubora zaidi tunapoheshimiana.

JITOLEE *kwa Utofauti, Tenda kwa Haki na Tumia tofauti zetu*
Tofauti zetu zinasaidia ubunifu na zinaweza kuleta bora ndani yetu. Mafanikio yetu yanategemea uwezo wetu wa kujifunza kutoka kwa nguvu na tofauti za mtu mwingine.

KUSHIRIKI *katika Mazungumzo Bora*
Wakati tunaongeza ubora wa mazungumzo, tunaboresha mahusiano, ubunifu, na matokeo.



Heshimu Ulimwengu Unaotuzunguka

HESHIMU *Jamii Zote*
Katika TNC, ushirikiano na jamii ulimwenguni kote hutuwezesha kutimiza wito wetu.

KUHESHIMU NA KUUNGA *Mkono Ukuzaji wa Haki za Binadamu*
Tunaelewa kuwa malengo na wito wetu havipaswi kuwa muhimu zaidi kuliko haki za watu wanaoishi katika jamii tunazozihudumia.

KUTENDA *kwa Uendeleu katika Kazi Yetu*
Kuhakikisha kuwa tunafanya kazi kwa njia endelevu kimazingira ni sehemu muhimu ya wito wetu wa Kuhifadhi Ardhi na Maji ambayo Maisha Yote Yanategemea.




Kutenda kwa Uadilifu

KUFUATA *Sheria na Kanuni Husika na Kuepuka Udanganyifu, Wizi na Rushwa*
Tunafuata sheria na kanuni husika ili kuhakikisha Uadilifu Usio na Lawama.

KUWA WATUMISHI WAZURI *kwa Fedha Zote za Mfuko na Wafadhili*
Tunatumia fedha za umma na za binafsi, kwa namna yoyote, kwa nia tu ya kuendeleza wito wa TNC.

KA SALAMA *na Waweke Wengine Salama*
Kwa kuzingatia hali ya kipekee ya kazi yetu katika TNC, tunawajibika kujiweka na kuwaweka wengine salama kwa uwanda mkubwa wa shughuli ulimwenguni.

EPUKA *Migongano ya Kimaslahi*
Katika TNC, tunaepuka migongano ya kimaslahi na dhana ya uwepo wa migongano ya kimaslahi.



Kuilinda TNC na Heshima Yake

JIHADHARI *na Mitandao ya Kijamii na Taarifa kwa Umma Zinazohusiana na TNC*
Ni muhimu tuzungumze wazi, kwa usahihi, na kwa uwazi kuhusiana na TNC na tuheshimu majukumu yetu kama wafanyakazi ili kulinda taarifa za siri.

KUDUMISHA *Hadhi Yetu ya Uhisani*
Kama mhisani wa umma, TNC inapata manufaa fulani, na vilevile majukumu muhimu. Ili kudumisha hadhi ya TNC, kazi yetu lazima iendeleze wito wetu.

KUWEKA TAARIFA ZA SIRI *Salama na Kuheshimu Faragha*
Ni wajibu wetu kuheshimu faragha ya mtu ambaye tunachakata taarifa zake binafsi. Aidha, lazima tuhifadhi taarifa zote za siri kuhusu kazi yetu kwa TNC zikiwa salama wakati wote.

KULINDA *Miliki ya Uvumbuzi*
Miliki yetu ya uvumbuzi hutusaidia kujitambulisha na kueleza sifa zetu kama shirika. Ni muhimu kuilinda.

KULINDA *Mali za TNC na Kutumia Mifumo ya Taarifa kwa Uwajibikaji*
Kama watumishi wa TNC, tunalinda mali zetu zisizohamishika na vilevile mali zetu kifedha na teknolojia na mifumo ya taarifa.

Maoni Yako Ni Muhimu

Tunakutegemea wewe kuuliza maswali na kutuarifu juu ya shaka za utovu wa nidhamu ili tuweze kufanya kazi kuzuia madhara dhidi ya wafanyakazi wetu, TNC na Wito Wetu.

Nenda kwenye [nature.org/codeofconduct](https://www.nature.org/codeofconduct) ili usome Kanuni zetu kamili.
Nenda kwenye [nature.org/tncchelpine](https://www.nature.org/tncchelpine) saa 24/7 ili kutoa taarifa za shaka.

Ninawezaje kutoa taarifa?

Ikiwa wewe ni mfanyakazi na una swali au unataka kuripoti wasiwasi juu ya ukiukaji wa Kanuni zetu au sheria, unaweza kuwasiliana na meneja wako, msimamizi mwingine wa TNC, mwanachama wa Timu ya Maadili na Utekelezaji au mwanachama wa Timu ya Watu wetu.

Wafanyakazi na wadau wengine wanaweza kuwasiliana na Timu ya Maadili na Utiifu kwa saa 24/7 kwa lugha tofauti kupitia [nature.org/tncchelpine](https://www.nature.org/tncchelpine) na unaweza kuficha utambulisho wako ikiwa utachagua hivyo.

Je, itakuwaje ikiwa mtu analipiza kisasi dhidi yangu kwa sababu nilitoa taarifa?

TNC haitavumilia ulipizaji kisasi dhidi ya watu ambao wanauliza maswali au kuibua shaka za ukiukaji wa Kanuni Zetu au sheria. Inahitaji ujasiri kulalamika. Tunaonyesha kujitoa kwetu kwa Maadili Yetu kwa kusaidiana wakati shaka na maswala yanapotokea.